



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Kwanza

KUSULIBIWA

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 27

Yuda Iskariote, aliyekuwa mmojawapo wa wanafunzi wa Yesu, ndiye aliyemsaliti Yesu. Yuda anafikiriwa kama mtu mwovu sana aliyepata kuishi kwa sababu ya kushiriki katika kifo cha Yesu. Wakati alipoanza kumfuata Yesu alifikiri ya kwamba Yesu angewafukuza Warumi katika nchi yao na kuanzia serikali mpya. Wanafunzi wengi wa Yesu pia walifikiri ya kwamba wakati jambo hilo lingefanyika, wangekuwa na kazi za madaraka katika serikali mpya. Wakati Yuda alipotambua ya kwamba Yesu hakutaka kuwa mfalme wa kidunia, alikata shauri kumsaliti kwa wakuu wa makuhani kwa vipande thelathini vya fedha. Unapoendelea kuisoma Biblia, utaona ya kwamba vipande hivyo vya fedha havikumfanya Yuda kuwa na furaha. Aliona ya kwamba tendo lile alilofanya lilikuwa kosa, na kwamba alitaka kuwarudishia wakuu wa makuhani vipande vile vya fedha. Soma Mathayo 27:3-8 kuona mambo yaliyompata Yuda na vipande vile vya fedha.

Pilato alikuwa liwali wa Kirumi wa Uyahudi katika wakati ule wa Yesu. Ilikuwa wajibu wake kuhukumu kesi muhimu zilizofanywa katika Uyahudi. Baada ya kumwuliza Yesu maswali, Pilato alisema ya kwamba Yesu hakutenda kosa lo lote. Walakini, aliogopa ya kwamba watu wangekasi-rika kama angemfungua Yesu. Kisha alikata shauri kufanya jambo ambalo lilionekana kuwa mpango mkuu. Wakati huo ulikuwa wa Pasaka kwa Wayahudi, na kila mwaka katika wakati huo ilikuwa desturi kwa liwali kumfungua mfungua mmoja.

Hakika, hii ilikuwa desturi lakini makuhani waliwaandea watu wakawashawishi kumwuliza Pilato kuwafungulia Baraba aliyekuwa mwizi na mwaaji badala ya Yesu. Watu walipiga kelele wakitaka Baraba afunguliwe. Halafu Pilato alisema, "Basi, nitafanya nini na mtu huyu aitwaye Yesu?"

Mkutano wa watu wale walipiga kelele, "Na asulibiwe. Na asulibiwe msalabani."

Pilato hakutaka kumwua Yesu, na kuonyesha jinsi alivyowaza moyoni mwake, alitwaa maji akanawa mikono yake. Wakati alipokuwa akinawa mikono yake aliwaambia watu wale, "Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki...." (Mathayo 27:24a)

Kisha mkutano wa watu wale walipiga kelele, "Na asulibiwe! Na asulibiwe msalabani!"

Pilato alijaribu tena kumwkoa Bwana. Aliwaambia askari wake kumpiga Yesu mijeledi, wakamvika vazi jekundu, wakasokota taji ya miiba, wakaiweka juu ya kichwa chake wakidhani ya kwamba kwa kufanya hivyo mkutano wa watu wale wangeweza kumhurumia Yesu. Askari hao walimdhiki, walisema, "Salamu, Mfalme wa Wayahudi!" (Mathayo 27:29b) Lakini mkutano wa watu wale hawakumwonea Yesu huruma bali walipiga kelele tena wakisema, "Na asulibiwe! Na asulibiwe msalabani!"

Hatimaye Pilato alikubali matakwa ya watu wale, akaamuru Yesu kusulibiwa msalabani.

Ilikuwa desturi katika nchi ile ya Uyahudi kwamba mtu alipohukumiwa kufa, ilikuwa lazima adhabu hiyo kutimizwa. Kwa hivyo, mara tu baada ya Pilato kutia sahihi yake kwa adhabu ya Yesu ya kifo, Yesu aliongozwa mpaka mahali pa kusulibiwa. Mahali hapa palikuwa mlimani nje ya mji wa Yerusalemu, na paliitwa Golgotha au Kalvari katika lugha ya Kirumi. Maana yake "Fuvu la Kichwa."



Yesu aliubeba msalaba wake akaanza kutembea kuelekea Golgotha akiwa amelindwa na kundi la askari wa Kirumi na kufuatwa na umati mkubwa wa watu. Walikutana na mtu mmoja Mkirene, jina lake Simoni. Mtu huyu alimsaidia Yesu kuubeba msalaba wake. Walipofika Golgotha, Yesu alisulibiwa msalabani katikati ya wanyang'anyi wawili ambao pia walisulibiwa.

Ilikuwa kama saa tatu asubuhi ambapo Yesu aliposulibiwa msalabani.

Ilipofika saa sita mchana, jambo lisilo la kawaida lilitokea. Palikuwa na giza juu ya nchi yote mpaka saa tisa alasiri.

Mama ya Yesu pamoja na wale wengine waliompenda Yesu

walikuwapo pale wakilia na kuomboleza kwa kifo cha Mwokozi mpendwa wao. Lakini maadui zake pia walikuwapo pale na walimdhaki wakisema, “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani.” Yesu alikuwa amenyamaza, kisha aliomba ombi fupi: “Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo.” (Luka 23:34)

Baada ya kifo cha Mwokozi, Yusufu wa Arimathaya alimwendea Pilato kumwomba mwili wa Yesu. Alijua kwamba, kwa kawaida, miili ya watu waliosulibiwa iliondolewa msalabani na kutupwa katika mahali pa takataka na kuliwa na wanyama na ndege. Pilato alimruhusu kutwaa mwili wa Yesu. Mwili wa Yesu ulitwaliwa kutoka msalabani, ukapakwa manukato. Kisha ulizongwa-zongwa katika sanda ya kitani safi, akauweka katika kaburi ambako mwili huu ulikaa siku tatu tu.

KAZI YA KUFANYA:

Andika namba ya mtu au watu wafuatao katika mistari iliyo kando ya sentensi hapo chini.

1. askari
2. Yuda
3. akida na askari wake wanne
4. Pilato
5. Yesu
6. mkutano wa watu
7. makuhani wakuu

— “Nalikosa nilipoisaliti damu isiyu na hatia.” (Mathayo 27:3)

— “Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu.” (Kifungu cha 54)

— “Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini.” (Kifungu cha 41-42)

— “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” (Kifungu cha 46).

— “Mnataka niwafungulie yupi? yule Baraba, au Yesu aitwaye Kristo?” (Kifungu cha 17)

— “Asulibiwe.” “Salamu, Mfalme wa Wayahudi!” (Vifungu 22, 29)

Chagua neno kutoka kwa orodha ya maneno yafuatayo na kulijaza katika nafasi iliyoachwa katika kila sentensi:

msalabani	fuvu la kichwa
Simoni	Yuda
	Pilato
askari	

1. Yesu alikufa _____ .
(Mathayo 27:40)
2. Liwali aliyemhukumu Yesu aliitwa _____ . (Mathayo 27:2)
3. _____ alimsaliti Yesu.
(Mathayo 27:3)
4. Yesu alisulibiwa na _____
wa Kirumi. (Mathayo 27:27)
5. Mlima ule ambapo Yesu alikufa
uliitwa Golgotha au _____ .
(Mathayo 27:33)
6. _____ Mkirene alisaidia
kuubeba msalaba wa Yesu.
(Mathayo 27:32)

Andika majibu ya maswali yafuatayo:

Yesu alitoa uhai wake ili kuwaokoa watu wote katika adhabu ya mauti ya milele kwa kutenganishwa na Mungu. Je! kwa nini watu wanahitaji kuokolewa? _____

Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya watu wote. Je, hii inamaanisha kwamba kila mtu ameokolewa? Je, ni hivyo au sivyo? _____



Ikiwa umekwisha kumwuliza Yesu kuwa Mwokozi wako, andika wakati na mahali ambapo ulifanya hivyo. _____

Ikiwa ungependa kumwomba Yesu kuwa Mwokozi wako sasa, andika sababu ya kutaka kufanya hivyo. _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi.”

1 Timotheo 1:15

Kifungu hiki kinaonyesha kwamba kulikuwa na maneno (au misemo) mengi kanisani. Neno lile lisemwalo hapa ni kwamba Yesu Kristo alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi. Neno hili, Paulo asema, lastahili kukubalika kabisa. Paulo asema, “wa kwanza wa wenye dhambi ni mimi.” Lakini dhambi zake alisamehewa bure kwa rehema ya Mungu. Mungu atamsamehe mtu ye yote atakayemwomba.



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Pili

UFUFUO

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 28

Siku ya kwanza ya juma ilikuwa ya ajabu sana. Yesu alikuwa amefufuka. Hadithi juu ya ufufuo katika Mathayo 28 inaanzia asubuhi na mapema siku ya tatu baada ya kifo cha Yesu msalabani. Wanawake wengine walikuja kaburini wakibeba manukato ya kupaka mwili wa Bwana uliokuwa umezongwa-zongwa katika kitani safi. Mariamu Magdalene ndiye aliyewaongoza wanawake wengine kwenda kaburini. Wakati walipokuwa wakitembea njiani walisemezana wao kwa wao, “Ni nani atakayetuingirishia lile jiwe mlangoni pa kaburi?” Kuhani alikuwa ameamuru kwamba jiwe kubwa livingirishwe mlangoni pa kaburi na kaburi lile kulindwa na askari kwa sababu alisikia kwamba wanafunzi na marafiki wa Yesu wanaweza kujaribu kuuiba mwili wa Yesu na kusema kwamba amefufuka katika wafu.

Wakati Mariamu Magdalene alipofika kaburini aliona ya kuwa lile jiwe lilikwisha kuvingirishwa, na askari

walikuwa wameondoka. Yeye pamoja na wenzake hawakujua kwamba kabla wao kuja kaburini Yesu alikuwa amekwisha fufuka. Kisha malaika wa Mungu alikuwa amekuja kutoka mbinguni akakalia jiwe lile mlangoni pa kaburi na sura yake ilikuwa kama umeme. Askari wa Kirumi waliogopa kwa yale waliyoyaona, wakakimbia. Mathayo anasema kwamba askari wale walinzi waliogopa sana wakatetemeka, wakawa kama wafu.



Lakini wakati Mariamu Magdalene na wanawake wale wengine walipofika kaburini waliona ya kuwa lile jiwe lilikwisha kuvingirishwa mbali na mlango wa kaburi. Malaika alisema nao. Aliwaambia, "Msiogope ninyi, kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa." (Mathayo 28:5-6) Kisha malaika aliwaambia kwenda upesi kuwaambia wanafunzi wa Yesu mambo hayo. Iliwapasa kwenda kuwaambia wanafunzi kwamba Yesu alifufuka katika wafu, na kwamba angewatungulia kwenda Galilaya ambako wagemwona. Walijua kwamba Bwana hakuwapo kaburini; na kwamba angewaona tena wanafunzi wake. Walitembea upesi kwenda Yerusalemu katika njia ile ambayo siku mbili tu zilizopita Yesu alikuwa amepitia kwenda Golgotha ambako alisulibiwa msalabani.

Walipofika katika mlango wa mji, walisimama kwa muda kuzungumza juu ya mahali ambapo wangekwenda kuwatafuta wanafunzi na kuwapasha habari za ufufuo wa Yesu. Walipokuwa wakiongea njiani, mtu mmoja aliwatokea. Mtu huyo alikuwa Yesu.

"Salamu!" Yesu aliwaambia.

Walimtambua, wakaogopa kwa sababu hawakufahamu jinsi alivyowatokea. Wakaanguka chini mbele zake. Yesu aliwahurumia akajaribu kuwafariji na kuwaongoza.

"Msiogope," Yesu aliwaambia. "Enendeni, mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoni-

ona." (Mathayo 28:10) Kisha alitoweka machoni pao. Hii ilikuwa mara ya pili kwao kuambiwa kwenda kuwaambia wanafunzi ya kwamba wagemwona Bwana Galilaya, nao walijiharakisha upesi kama Yesu alivyowaamuru.

Askari walinzi waliokuwa wakilinda kaburi walikwenda upesi mjini wakawapasha wakuu wa makuhani habari. Pilato alikuwa amewaweka walinzi hao chini ya amri ya wakuu wa makuhani, na walijua kwamba adhabu ya serikali ya Rumi kwa kitu cho chote kinacholindwa kikitoweka ni kifo tu kwa walinzi. Labda walifikiri kwamba habari yao juu ya tetemeko kubwa la nchi na juu ya malaika ingepokewa zaidi na viongozi wa dini kuliko Pilato. Wakuu wa makuhani walikusanyika pamoja na wazee wakafanya mipango. Waliwapa askari pesa nyingi wakisema, "Semeni, ya kwamba wanafunzi wake walikuja usiku, wakamwiba, sisi tulipokuwa tumelala. Na neno hili likisikikana kwa liwali, sisi tutasema naye, nanyi tutawaondolea wasiwasi." Askari wale walinzi walipokea pesa wakafanya mambo waliyoambiwa.

Baada ya siku ya ufufuo, siku arobaini zilipita, na katika siku hizo Yesu alisema mara kwa mara na wanafunzi wake kuhusu ufalme wa Mungu. Wanafunzi wale kumi na mmoja walikwenda mlimani Galilaya ambako Yesu aliwaambia kwenda.

Wakati walipomwona, walimsujudia ingawa baadhi yao waliona shaka. Yesu aliwaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;

na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” (Mathayo 28:18-20)

KAZI YA KUFANYA:

Je! ni nani anayesema kwamba kaburi lilikuwa tupu? _____

Tulijuaje kweli kwamba lilikuwa tupu? Jaza nafasi zilizoachwa kwa majibu ya maswali yafuatayo. Unaweza kupata majibu kwa kusoma vifungu vya Biblia.



Soma Mathayo 28:1-4.

1. Je! wakati _____
walipokuja kaburini asubuhi na
mapema walipata nini? _____

Soma Mathayo 28:5-7.

2. Je! _____ alisema
kwamba kulifanyika nini? _____

Soma Mathayo 28:11-15.

3. Je! Mkuu wa makuhani alimwambia
kila _____ kusema
kwamba kulifanyika nini? _____

4. Je! tunahitaji kufanya nini kupata
uzima baada ya kufa? _____

Soma sasa ukweli wa uzima wa milele na kuwa tayari darasani kueleza baadhi ya mambo uliyofikiria wakati ulipokuwa ukisema juu ya uzima wa milele.

Yesu alisema, ...“Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi.”

Yohana 11:25

“Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima,...hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Yesu Bwana wetu.” Warumi 8:38-39

“...Heri wafu wafao katika Bwana...”

Ufunuo 14:13

“Maana ikiwa tunaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.... Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni...na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.”

1 Wathesalonike 4:14, 16-17

“Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.” Ufunuo 21:4

“Nao watamwona uso wake.... Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa waia nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele.” Ufunuo 22:4-5

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“...nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.” Ufunuo 1:18

Yesu alikuwa akisema katika kifungu hiki kwamba yeye ndiye yule aliyesulibiwa, na aliyekufa, lakini sasa yuko hai milele na milele. Funguo ni ishara ya mamlaka. Kristo aliye hai, na aliye na uhai ndani yake mwenyewe, na aliye chanzo cha uhai kwa wengine, ana mamlaka duniani na mbinguni.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Tatu

KUWA MMOJAWAPO WA JAMAA YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 3:1-21

Wakati ulikuwa umefika tena kuadhimisha sikukuu ya kila mwaka ya Pasaka. Makundi ya watu walitoka katika kila sehemu ya nchi kuja kuadhimisha sikukuu hii ya kidini.

Baada ya sikukuu hii, Yesu alianza kuwafundisha watu na kufanya miujiza kati yao. Watu wengi walimwamini waliposikia maneno yake na walipoona kazi yake ya ajabu ambayo mtu ye yote hangeweza kufanya.

Mmojawapo wa watu waliomwamini Yesu alikuwa mkuu wa Wayahudi. Aliitwa Nikodemo, na alikuwa tajiri sana. Palikuwepo na Mafarisayo wengi kati ya wakuu wa Wayahudi. Watu hawa walijivuna sana na hawakutaka kuwapokea Yohana Mbatizaji au Yesu kama waalimu waliotoka kwa Mungu. Wao wenyewe walitamani kuwa viongozi wa dini ya Wayahudi na waliwadharau watu wanyenyekevu kama Yohana na Yesu. Lakini Nikodemo hakuwa na tabia kama ya

watu hawa. Alimsikia Yesu akiwafundisha watu waliokuja kuadhimisha sikukuu ya Pasaka, akaamini kwamba kweli alikuwa mkuu.

Wakati Mafarisayo wengine walipokuwa wakijaribu kumtoa Yesu makosa, Nikodemo alitamani kusikia mafundisho yake mengi. Hata siku moja usiku alimjia Yesu wakati alipokuwa Yerusalemu, akamwomba kuzungumza naye.

Yesu alimpokea Nikodemo kwa furaha na alizungumza naye juu ya ufalme wa Mungu. Alimwambia kwamba mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuona ufalme wa Mungu. Nikodemo alistaajabu sana jinsi jambo hili lingewezekana, kwa hivyo Yesu alimweleza siri ya kuzaliwa mara ya pili ambayo tunaita badiliko la roho. Mkuu huu wa Wayanudi alikuwa hajapata kamwe kusikia maneno haya ya ajabu, na alimsikiliza Yesu kwa kustaaajabu wakati Yesu alipokuwa akimsimulia juu ya upendo mkuu wa Mungu. Yesu alisema ya kwamba upendo huu

ulimfanya Mungu kumtoa Mwanawe pekee ili kila mtu asife kwa ajili ya dhambi, bali awe na uzima wa milele.



Kisha Yesu alimkumbusha Nikodemo hadithi ya Musa alipokuwa jangwani ambapo wana wa Israeli walitenda dhambi na Mungu akawatuma nyoka katika kambi yao. Nikodemo alikumbuka hadithi hiyo na Yesu akasema, “Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa.” (Yohana 3:14) Nikodemo hakufahamu ya kwamba Yesu alikuwa akizungumza juu ya njia ya ukatili ambayo angesulibiwa siku moja ili kuwaokoa watu katika dhambi zao. Lakini Nikodemo aliamini kabisa ya kwamba Yesu alikuwa mwalimu mkuu aliyetoka mbinguni kukaa na watu.

Haya ndiyo yaliyokuwa mazungumzo yao:

Nikodemo: “Twajua ya kuwa u mwalimu umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye. (Yohana 3:2)

Yesu: “Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.” (Yohana 3:3)

Nikodemo: “Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili na akazaliwa?” (Yohana 3:4)

Yesu: “Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, hamna budi kuzaliwa mara ya pili. Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.” (Yohana 3:7,8)

Nikodemo: “Yawezaje kuwa mambo haya?” (Yohana 3:9)

Yesu: Je! unakumbuka jinsi Mungu alivyowaokoa Waisraeli jangwani wakati walipoumwa na nyoka iliokuwa na sumu? Alimwambia Musa kutengeneza fimbo ya nyoka ya shaba na kuiinua juu. Watu waliomwamini Mungu kuwaokoa walitazama fimbo ile ya nyoka ya shaba, wakaponywa. Vile nyoka wa shaba alivyoinuliwa juu, vivyo hivyo Mwana wa Mungu atainuliwa juu ya msalaba. Kila mtu anayemwamini atakuwa na uzima wa milele.

KAZI YA KUFANYA:

Tunapokeaje uzima mpya wa Mungu? Soma Yohana 3:3 na 3:16. Chora mviringo kwa namba ya kila jibu lililo kweli.

1. Kwenda kwa Shule ya Jumapili.
2. Kumwamini Yesu.
3. Kusoma Biblia yangu.

4. Kwa kuzaliwa mara ya pili.
5. Kutosema uwongo, kutoapa, kutodanganya, au kutopigana.



Je! umepata kufikiria kama Mungu ana jamaa? Tambua mafanikio ya kuwa katika jamaa ya Mungu. Soma vifungu vya Biblia. Tafuta maneno utakayojaza katika nafasi zilizoachwa hapo chini.

Maisha Mapya: Soma 1 Yohana 5:11-12

“Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.”

Mungu anatupa uzima wa _____
Wale wanaoliamini jina la _____
wanajua kwamba wana uzima wa Mungu.

Jamaa Wengi: Soma Wagalatia 3:26 kuona jinsi Wakristo wanavyohusiana na Mungu.

“Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa

wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo.”

Jaza nafasi ifuatayo:

Sisi sote ni _____ wa Mungu.

Sasa soma Warumi 8:15 kuona jinsi Mungu anavyohusiana sisi wenyewe katika jamaa ya Mungu.

“Kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, aba, yaani, Baba.”

Jaza nafasi ifuatayo:

Yeye ni _____ yetu.

Sasa soma 1 Yohana 3:14 kuona jinsi tunavyohusiana katika jamaa ya Mungu.

“Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mautini kuingia uzimani kwa maana twawapenda ndugu.”

Jaza nafasi ifuatayo:

Sisi ni _____

Jina Maalum: Unapokuwa mmojawapo wa jamaa ya Mungu, unapewa jina jipya. Soma Waefeso 3:14, 15.

“Kwa hiyo nampigia Baba magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa.”

Jaza nafasi ifuatayo:

Jamaa ya Mungu huitwa kwa _____ lake.

Nafasi Maalum: Soma Wafilipi 4:19 kuona jinsi Mungu anavyotunza watoto wake.

“Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.”

Jaza nafasi zifuatazo:

Mungu anatupa _____ yetu
yote kadiri ya _____ wake.

Soma Warumi 8:17 kuona habari za urithi.

“Na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo...”

Jaza nafasi ifuatayo:

Wewe ni _____ wa
Mungu.

Wajibu Maalum: Soma Yereimia 7:23.

“Lakini naliwaamuru neno hili, nikisema, sikilizeni sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu, mkaende katika njia ile yote nitakayowaamuru, mpate kufanikiwa.”

Jaza nafasi zifuatazo:

Wale ambao ni wa Mungu _____
sauti yake na _____ katika
njia yote _____.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.”

Yohana 3:3

Tunazaliwa “mara ya pili” kwa kumwamini Yesu Kristo kama Mwokozi wetu. Huu ni uzazi wa

kiroho. Tunaweza kupokea maisha mapya yanayotufanya kuwa watu wema wenye njia mpya. Hakika, miili yetu haibadiliki. Kwa uso wetu tunaonekana kama tulivyo sikuzote, lakini ndani tunapokea maisha mapya tunapozaliwa mara ya pili. Tunakuwa watoto wa Mungu walio na maisha ya Mungu na tunataka kufuata njia za Mungu. Kisha tunakuwa katika jamaa ya Mungu. Tuna uchaguo. Tunaweza kuchagua kuzaliwa mara ya pili au kukaa kama tulivyo.

Je! umekwisha kuchagua kupokea maisha ya Mungu na kuwa mmojawapo wa jamaa yake?



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI

KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Nne

KUKAA KATIKA JAMAA YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 4:1-41

Katikati ya Uyahudi na Galilaya palikuwa na nchi moja ndogo iliyoitwa Samaria. Watu wa Samaria walikuwa maadui wakubwa wa Wayahudi, na wakati ule wa Yesu walikuwa bado wakichukiwa sana na Wayahudi. Ingawa Yesu alikuwa Myahudi, hakuwa na chuki na watu wa Samaria walioitwa Wasamaria. Yesu hakukataa kupitia nchi yao alipokuwa safarini kurudi kwao Nazareti.

Kwa sababu Yesu alitaka kufuata njia fupi kupitia Samaria, wanafunzi wake pia walikubali kufuata njia hiyo ili kuwapo pamoja naye. Kwa hivyo, walisafiri pamoja hadi walipofika katika mji mmoja mdogo ulioitwa Sikari.

Karibu na mji huo palikuwa na kisima ambacho kilichimbwa miaka mingi sana iliyopita, pengine kilichimbwa na Yakobo mjukuu wa Ibrahimu. Na kwa heshima yake, kisima hiki kilikuwa bado kikiitwa

kisima cha Yakobo. Walipofikia kisima hiki, Yesu alikuwa amechoka. Aliketi kando yake kupumzika baada ya kusafiri safari yake ndefu. Wanafunzi wake walikwenda mjini kununua chakula, wakamwacha peke yake pale kisimani.

Mwanamke mmoja wa pale Sikari alifika kisimani kuteka maji. Alimwalia mgeni (Yesu) aliyekuwa ameketi kando ya kisima, akaona kwamba alikuwa Myahudi kwa kuwa alijua kwamba Wayahudi hawakujali Wasamaria, alimpita Yesu, akajiharakisha kuteremsha chombo chake kisimani kwa kamba ndefu. Alikuwa tayari kuanza mwendo kurejea mjini, Yesu akamwomba maji ya kunywa.

Kwa kushangaa kwa ombi hilo, mwanamke yule alijibu, "Imekuwaje wewe Myahudi kutaka maji kwangu, nami ni mwanamke Msamaria? (maana Wayahudi hawachangamani na Wasamaria)." (Yohana 4:9)

Yesu alijibu, akimwambia, "Kama ungalijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, Nipe maji ninywe, ungalimwomba yeye, naye angalikupa maji yaliyo hai." (Yohana 4:10)

Maneno hayo yaliamsha tamaa ya mwanamke yule mara moja. "Mgeni huyu ni nani?" alijiuliza. Aliona kwamba mgeni huyu alikuwa na mawazo tofauti na ya Wayahudi wengine kwa kuwa Wayahudi wengine waliona ni heri kuteseka kuliko kusema na Msamaria. Kwa hivyo, alisema, "Bwana, huna kitu cha kutekea, na kisima ni kirefu; basi umeyapata wapi hayo maji yaliyo hai? Je! wewe u mkubwa kuliko baba yetu, Yakobo, aliyetupa kisima hiki, naye mwenyewe akanywa maji yake, na wanawe pia, na wanyama wake?" (Yohana 4:11-12)

Yesu akajibu, "Kila anywaye maji haya ataona kiu tena; walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele." (Yohana 4:13-14)

Sasa mwanamke yule alikuwa akisikiliza kwa makini. Hakujua kwamba maji yaliyo hai ambao Yesu alizungumza habari yake yalikuwa kipawa chake cha wokovu anachotoa bure kwa watu wote, kwa hivyo alisema, "Bwana, unipe maji hayo, nisione kiu, wala nisije hapa kuteka." (Yohana 4:15)

Yesu alifurahi kwamba mwanamke yule alipendezwa. Alianza kusema naye juu ya dhambi zake. Alijua kwamba mwanamke yule alikuwa mwenye dhambi sana, na alimwambia mambo mengi maovu ambayo alifanya. Mwanamke yule alistaajabu sana jinsi

Yesu alivyoweza kujua mambo hayo. Ilionekana kama kwamba Yesu alijua fikira zake zote. "Bwana, naona ya kuwa u nabii," alimwambia Yesu.

Ingawa mwanamke yule alikuwa mwenye dhambi, alistaajabu mara nyingi ikiwa kweli Mungu alipendezwa zaidi na dini ya Wayahudi kuliko dini yao ya Wasamaria. Sasa alimwuliza Yesu kama iliwapasa watu kuabudu katika Yerusalemu au katika hekalu la Wasamaria.

Yesu alimjibu ya kwamba Mungu alipanga kuleta wokovu kupitia taifa la Wayahudi, lakini alisema wakati ulikuwa umefika ambapo waabudu kweli hawakuhitaji kwenda tena Yerusalemu kwa kuwa wangemwabudu Mungu mahali po pote. Alisema, "Mungu hayupo mahali pamoja. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kuamini kwamba yeye ni Roho."

Kisha mwanamke yule alisema, "Najua ya kuwa yuaja Masihi, (aitwaye Kristo); naye atakapokuja, yeye atatufunulia mambo yote." (Yohana 4:25)

"Mimi ninayesema nawe, ndiye," Yesu alisema, na mwanamke yule alionyesha uso wa furaha, akamstaajabia Yesu. Lakini wakati ule ule wanafunzi wa Yesu walirudi kutoka mjini, wakaleta chakula, kwa hivyo mwanamke yule aliacha mtungi wake, akaenda mbio mjini kuwaambia marafiki zake habari za mtu huyu wa ajabu (Yesu) ambaye alimkuta kisimani.

Wanafunzi walistaajabu kwa nini Yesu alisema na mwanamke Msamaria lakini hawakumwuliza swali lo lote. Walimletea chakula na alipokataa

walimsihi kula. Kisha aliwaambia, "Mimi ninacho chakula msichokijua ninyi." (Yohana 4:32) Waliulizana, "Je! mtu amemletea chakula?" (Yohana 4:33) Lakini Yesu alijua maswali hayo yao, kwa hivyo alisema, "Chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake." (Yohana 4:34)

Mwanamke yule alipofika mjini aliwaambia watu habari za Yesu aliyemwambia mambo yote aliyotenda maishani mwake. "Aliniambia mambo yote niliyoyatenda." (Yohana 4:39b) Je! haimkini huyu kuwa ndiye Kristo?" aliuliza. Watu wale walikata shauri kwenda kumwona mtu huyu wao wenyewe, kwa hivyo walikwenda pamoja naye katika kisima kile cha Yakobo.

Yesu alizungumza na Wasamaria kuhusu mambo ya Mungu, na walimkaribisha kukaa kwao kuwafundisha mambo haya ya ajabu. Alikaa huko Sikari siku mbili akiwafundisha watu. Halafu aliondoka huko, akaenda Nazareti na kuwaacha waamini wengine kati ya Wasamaria.

KAZI YA KUFANYA:

Pata Uzima Mpya: Mwanamke yule Msamaria alipata maisha mapya. Soma vifungu vya Biblia vifuatavyo na kujibu maswali kwa kuchora mviringo kwa namba iliyo kando ya jibu lililo kweli.

Je! kwa nini tunahitaji kuwa tofauti? Mungu anatupa picha inayoonyesha jinsi kila mtu ulimwenguni alivyo. Tusome Zaburi 53:3. "Kila mtu amepotoka, wameoza wote pamoja, hakuna atendaye mema."

Je! kifungu hiki kinatwambia kwamba tumefanana na nini?

1. Watu wengine ni wema.
2. Hakuna hata mmoja wetu mwenye haki mbele za Mungu.

Je! ninaweza kupata uzima mpya? Ingawa sisi sio wema wa kutosha kwa Mungu, anaahidi kwamba tunaweza kupata uzima mpya. Tusome habari hii katika 2 Wakorintho 5:17. "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya."

Je! Mungu anaahidi kwamba kitu gani kitapita?

1. Kila kitu kinachotufanya kutokuwa na furaha.
2. Mambo ya zamani tuliyozoea kufanya na kufikiria.

Je! kitu gani ambacho Mungu anasema kinakuwa kipya na tofauti?

1. Tunapata sheria za kufuata katika kuishi.
2. Tunakuwa na njia mpya za kutenda mambo na kufikiri.

Je! uzima huu mpya unatoka wapi? Mungu pekee ndiye anayeweza kutupa uzima huu mpya. Yohana wa Kwanza 5:11-13 inatuambia habari zake.

Je! ni uzima gani Mungu anautoa?

1. Uzima wa malaika.
2. Uzima wa mtoto.
3. Uzima wa milele.

Je! Mungu anatoa uzima wake kwa nani?

1. Mungu anatoa uzima huu kwa watu wema pekee.
2. Mungu anatoa uzima wake kwa wale wanaomwamini Yesu Kristo Mwanawe.

Tunapokeaje uzima mpya wa Mungu? Tukitaka kufahamu jinsi tunavyopokea uzima mpya, tunahitaji kujua kwanza jinsi hatuwezi kuupokea. Soma Waefeso 2:8,9.

Je! maana yake nini kwamba hatuwezi kuokolewa katika dhambi kwa “kazi” tunazofanya?

1. Hatuwezi kuondoa uzima wa dhambi kwa kutenda matendo mema.
2. Hatuwezi kuondoa dhambi zetu kwa kupokea pesa.

Mungu anatwambia katika Yohana 3:16 na 1:12 hasa jinsi tunavyoweza kupokea uzima wake mpya.

Tunapokeaje kipawa cha Mungu cha uzima?

1. Tunapokea kipawa cha Mungu kwa kazi zetu.
2. Tunapewa kipawa cha Mungu wakati tunapompokea Yesu kuwa Mwokozi wetu.

Je! uzima wa Mungu unafanya tofauti gani ndani yetu? Tunapompokea Yesu kama Mwokozi wetu katika dhambi, tunapata kipawa cha Mungu cha uzima na tunazaliwa katika jamaa yake. Ni uzima wake ndio unaotufanya kuwa watu wapya walio na nia ya kuishi kulingana na maongozi ya Mungu. Unapokwisha kupata uzima wa Mungu ndipo utakapobadilika.

Je! ninaonyesha Uzima Mpya wa Mungu? Weka alama hii (✓) katika mistari iliyo kando ya sentensi zinazonyesha jinsi unavyoona moyoni na unavyofikiri.

1. — Marafiki zangu wasipoecheza mchezo ninaopenda sichezi.
2. — Nafikiri si haki mimi kuifanya kazi nyingi zaidi kuliko ndugu au dada yangu mdogo.
3. — Nafikiri si haki kwamba siwezi kufanya mambo ambayo ndugu au dada yangu mkubwa anafanya.
4. — Ni haki kuwa mbaya kwa mtu mwingine ikiwa mtu huyo ni mbaya kwako.
5. — Unaweza kuiba vitu ikiwa una ujanja kutokamatwa.
6. — Ninasema uwongo mara moja tu baada ya siku nyingi kama uwongo huo utanifanya kutoingia taabuni.
7. — Sitaki kulaumiwa, kwa hivyo ninatoa udhuru au ninamlaumu mtu mwingine.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.”

Warumi 6:23

Jaribu kujifunza kifungu hiki kukusaidia kuwaeleza marafiki zako uzima mpya ambao Mungu anatoa kwa kila mtu. Dhambi hutuzwa mauti; lakini uzima wa milele hatupokei kwa matendo yetu, bali tunapewa bure kwa rehemu ya Mungu. Kuna tofauti kati ya mishahara na karama. Mishahara ni malipo mnayopokea kwa kutenda kitu kinachostahili kulipwa. Karama ni kitu mnachopokea bure bila kutenda kazi yote au kitu cho chote kinachostahili karama.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Tano

KUWA NA FURAHA KATIKA JAMAA YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Luka 15:11-32


Wakati Yesu alipokuwa akifundisha katika Perea, sehemu ya mwisho ya nchi ya Israeli iliyompassa kuitembelea, aliwaambia watu mfano juu ya Mwana Mpotevu. Mpotevu maana yake ni mtu anayetapanya mali, na mwana huyu alitapanya mali.

Luka anatwambia kwamba watoza ushuru wengi na wenye dhambi walimfuata Yesu kusikia maneno yake. Na Mafarisayo na waandishi wakampata kuwa na hatia. Yesu alijua jinsi walivyokuwa wakinung'unika juu yake, akasema na watu kwa mifano.

Yesu alisimulia hadithi hii kwa kusema kwamba mtu mmoja alikuwa na wana wawili; mwana mdogo hakutosheka na kukaa nyumbani pamoja na baba na ndugu yake. Alimwambia baba yake kumpa sehemu ya urithi wake. Baba yake alimgawia pesa, akachukua pesa hizo. Alitumia pesa hizo katika kila anasa, na alikuwa na marafiki wengi. Lakini baada ya

muda mfupi alitumia pesa zake zote, akabaki bila kitu. Kisha aliona njaa na marafiki zake wakamwacha, wakakataa kumsaidia.

Katika taabu yake, mwana huyu alijitoa kulisha nguruwe, lakini hakuweza kuzuia kuteseka. Hakuna mtu aliyemhurumia, au aliyempa chakula.



Kisha mwana huyu alikumbuka baba yake na watumishi waliotumika nyumbani mwa baba yake. Alijua kwamba watumishi hao walilishwa vema. Alikata shauri kurudi kwa baba yake na kumwuliza kumfanya kama mmoja wa watumishi wake.

Baba yule alimpenda sana mwana huyu wake mpotevu, na alikuwa na

huzuni wakati mwana huyu alipoondoka nyumbani kwenda kukaa katika nchi ya mbali. Kila siku alitamani mwana huyu arudi nyumbani. Hatimaye alipomwona akija, kama amevaa nguo zilizoraruka, alikimbia kwenda kumlaki, akalia



machozi kwa furaha. Mwana huyu alianza kuzungumza. Alisema, “Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako.” (Luka 15:21) Lakini hakupata nafasi kumweleza baba yake jinsi alivyotaka kuwa kama mmoja wa watumishi wake kwa sababu kabla yeye kusema zaidi baba yake alimwamuru mtumwa kuleta upesi vazi lililo bora na kumvika, na kuandaa karamu kwa kuwa mwanawe huyu aliyekuwa amepotea sasa alionekana.

Mwana mkubwa alikuwako shambani akifanya kazi. Wakati aliporudi nyumbani na kusikia sauti za nyimbo na michezo, aliwauliza watumishi mambo yaliyofanyika. Walimwambia kwamba ndugu yake

mdogo alikuwa amekuja. Alikasirika, akakataa kuingia ndani ya nyumba kumwona nduguye. Kisha baba yake alitoka nje, akamwambia habari njema kuhusu ndugu yake, lakini bado aliendelea tu kukasirika. Alisema, “Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wo wote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu; lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinja yeye ndama aliyenona.” (Luka 15:29-30)

Baba yao alifahamu sasa ya kwamba mwanawe mkubwa alikuwa akimwonea wivu ndugu yake. Alimwambia, “Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.” (Luka 15:31-32)

Watu wa wakati ule wa Yesu na nchi yao, waliheshimu sana sheria. Waliona ya kwamba ilikuwa lazima kuishi kwa sheria, na kwamba ilipasa watu kutuzwa au kuadhibiwa kulingana na jinsi walivyofuata sheria ya jamii yao.

Yesu aliheshimu sheria na desturi za watu wake, lakini alikuwa na ujumbe mpya aliotaka kuwapa wanadamu, na ujumbe huo haukuwa na sheria ndani kuhusu matendo. Ulikuwa ujumbe wa furaha kwamba upendo wa Mungu kwa kila mtu hauna mwisho. Hata kama mtu ni mbaya jinsi gani, upendo wa Mungu upo kwake ikiwa tu atajitoe mwenyewe kwa Mungu kwa moyo wake wote. Kwa kutaka kufundisha ukweli huu mkuu kwa wasikilizaji

wake, Yesu alijifikiria na watu kwa kusudi tu kwamba alikuwa akijaribu mawazo yao juu ya mambo waliyofikiria kuwa haki.

KAZI YA KUFANYA:

Fikiria majibu ya maswali yafuatayo. Usiandike majibu, bali kuwa tayari kuyajibu wakati mwalimu wako anapokuuliza.

1. Je! kulikuwa na ubaya wote kwa mwana yule kuondoka nyumba ikiwa alikuwa mkubwa kutosha?

2. Je! mwana yule alifanya jambo la busara kukubali kwamba njia yake ilikuwa mbaya?

Je! ipi ingehitaji ujasiri mwingi, kuficha hali iliyompata na makosa au kukubali na kujaribu kusawazisha makosa?

3. Je! watu gani wanafanana na mwana yule?

4. Je! wewe kama Mwana wa Mungu, kuna wakati wote unapojiona kuwa mbali sana na Mungu ingawa wewe ni mmojawapo wa jamaa yake?

5. Je! kwa nini hatujioni kuwa karibu na Mungu wakati tunapotenda dhambi?

6. Mimi kama mtoto wa Mungu nawezaje kusawazisha mambo kati yangu na Mungu?

Furaha katika Jamaa ya Mungu: Mungu amekwisha kutuonyesha jinsi ya kusawazisha mambo katika jamaa yake. Soma kila swali lililo hapo chini. Kisha tafuta majibu katika vifungu vya Biblia vilivyo chini ya kila swali. Tafuta

maneno yaliyo katika ukurasa ufuatao ambayo yanafanana na maneno uliyosoma katika kifungu cha Biblia. Andika herufi ya maneno hayo katika mstari ulio kando ya kifungu cha Biblia.

1. Tunathibitishaje kwamba tunamjua Mungu?

— 1 Yohana 2:3-4 “Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, Nimemjua wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake.”

2. Ushirika wetu na Mungu unakuwaje tunapotenda dhambi?

— Isaya 59:2 “Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu.”

3. Ni nani atakayetuomba tunapotenda dhambi?

— 1 Yohana 2:1 “Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki.”

4. Je! Mungu huwaza nini wakati tunapotenda dhambi?

— Zaburi 86:15 “Lakini Wewe, Bwana, U Mungu wa rehema na neema.”

5. Je! inatupasa kuwaza wakati tunapotenda dhambi?

— Yakobo 4:10 “Jidhilini mbele za Bwana, naye atawakuza.”

6. Tunawezaje kuwa na furaha tena katika jamaa ya Mungu?

— 1 Yohana 1:9 “Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.”

- A. Inatupasa kujinyenyekeza na kuhuzunika kwamba tuko mbali na Mungu kwa sababu ya dhambi.
- B. Ingawa Mungu anachukia dhambi, anatupenda, na anavumilia kutonyesha rehema tunapoacha dhambi.
- C. Yesu aliyekufa kwa ajili yetu atakuwa mwombezi wetu kwa Baba yake.
- D. Jamaa ya Mungu huthibitisha ushirika wa jamaa yake kwa kutaka kutii Neno la Mungu.
- E. Ni lazima tutubu dhambi tuliyo-fanya, kisha Mungu atatusamehe.
- F. Mungu anatupenda sana, lakini wakati tunapotenda dhambi, tunatengwa naye.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu... Unirudishie furaha ya wokovu wako.”

Zaburi 51:10, 12a

Mkristo anataka kuwa na furaha katika jamaa yake hapa ulimwenguni. Anataka pia kuwa na furaha katika jamaa ya Mungu. Wakati tunapotenda dhambi, tunakosa kuwa na furaha. Tunajua kwamba Baba yetu pia hana furaha. Hapo zamani Mfalme Daudi alitambua jambo hili kuwa kweli. Kifungu hiki cha Zaburi ni maombi ambayo Daudi aliomba.

Je! unafikiri Mfalme Daudi alikuwa na maana gani aliposema:

“Moyo safi” _____

“Roho iliyotulia” _____

“Furaha ya wokovu” _____

Maombi haya ni muhimu sana kukumbuka. Labda tunaweza kuomba hivyo wakati tunapotenda jambo baya.



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

Sura ya Sita

KUSUDI LA MUNGU KWA MUSA

MASOMO YA BIBLIA: Matendo
7:17, 20-22

Ulikuwa wakati wa huzuni kwa Waebrania. Walikuwa watumwa katika nchi ya Misri. Mfalme Farao aliogopa kwamba idadi ya Waebrania hao ingeongezeka na kwamba wangepindua serikali yake. Kwa hivyo, aliamuru kwamba watoto wote wanaume waliozaliwa na wanawake wa Kiebrania wauawe.

Ulikuwa wakati wa huzuni, wakati mtoto Musa alipozaliwa. Wazazi wake walimficha kwa muda wa miezi mitatu nyumbani mwao. Waliogopa kwa sababu askari wa Farao walikuwa wakiwatafuta watoto wa Kiebrania kila mahali kuwaua.

Mama yake Musa alipokuwa hawezi kumficha tena, alifanya kisafina cha manyasi. Alifanya kisafina hicho kwa uangalifu sana hata hakikuweza kuvuja. Alipomaliza kukifanya, alimtia mtoto Musa ndani, akakiweka kando ya Mto wa Nile kuelea. Alimwacha

Miriamu, dada ya Musa, kumlinda ili kuona yale yatakayompata.



Baadaye binti Farao pamoja na wajakazi wake walikuja kuoga pale mtoni. Aliona kisafina kile, akasikia mtoto akilia ndani. Alimtuma mjakazi wake mmoja kwenda kukileta, akakifungua, akamwona mtoto Musa. Alimchukua kuwa wake. Miriamu alitoka katika mahali alipojificha, akaja mara moja, akamwuliza binti Farao kama alihitaji mlezi ambaye angemlea mtoto yule. Alikwenda mara moja



kumwita mama yao, akaja naye. Kisha Musa na mamaye wakapelekwa na binti Farao kukaa katika makao ya mfalme. Mamaye Musa alimlea. Pia aliweza kumfundisha habari za kabila lao na za Mungu. Aliomba ya kwamba siku moja Musa angeweza kuwaokoa watu wake katika utumwa.

Tunaambiwa katika Matendo 7:22 kwamba Musa alikuwa mwanafunzi mwema. Alijifunza hesabu, elimu ya nyota, historia, sheria, kusoma na kuandika. Pia alijifunza kupiga upindi na mambo ya vita.

Hapakuwapo wasichana katika shule Musa aliyosomea wala vijana maskini au vijana wa jamaa za Kiebrania. Elimu katika Misri ilikuwa kwa watoto wa jamaa ya kifalme na wa matajiri peke vao.

Je! unafikiri ni ajabu kwamba Musa alitiwa ndani ya kisafina cha manyasi na baadaye akakaa katika makao ya Mfalme? Mungu alikuwa na

kusudi kwa maisha yake. Katika kusudi hili, Musa angehitaji kutumia elimu yote na mambo aliyojifunza.

Njia moja ambayo Musa alitumia elimu yake inapatikana katika Kutoka 24:4, “Basi Musa akayaandika maneno yote ya Bwana.”

Hakika, Musa alikuwa akiwafikiria watu wake wakati alipokuwa akisoma katika shule iliyokuwa katika makao ya Mfalme. Baadaye aliwachunga kondoo za mkwe wake. Alijifunza hali ya jangwa.

Katika kila mojawapo wa nyakati hizi alisema na Mungu na alijifunza mambo yote ambayo angehitaji ili kutimiza kazi kubwa ya Mungu.

Je! unashukuru kwa ajili ya Shule yenu? Watu wengi hawapati nafasi ya kwenda shuleni. Inakupasa kujifunza mambo yote unayoweza ili uweze kutimiza kusudi maalum ambalo Mungu analo kwa maisha yake.

KAZI YA KUFANYA:

Hapo chini pameandikwa kweli fulani juu ya watu walio katika somo hili letu. Picha ya kila mtu iko upande wa kulia. Chagua picha inayolingana na kweli hizo na kuandika namba yake kwenye mstari ulio mbele ya swali “Je! Mimi Ni Nani?”

Nilizaliwa katika nyumba ya Kiebrania. Nilitiwa ndani ya kisafina cha manyasi, nikawekwa kando ya Mto Nile. Nilikaa katika makao ya Mfalme.

Je! mimi ni nani?

Nililinda kisafina cha ndugu yangu mtoni. Nilimleta mama yangu kumlea

Musa katika makao ya mfalme.

Je! mimi ni nani?

Siku moja nilikwenda mtoni kuoga nikapata kisafina cha manyasi. Nilileta mtoto wa Kiebrania kukaa katika makao ya Mfalme.


Je! mimi ni nani?

Nilimficha mtoto wangu nyumbani kwa miezi mitatu. Nilifanya kisafina cha manyasi nikamtia ndani, kisha nikakiweka kando ya mto. Baadaye nikawa mlezi wake katika makao ya mfalme. Niliweza kumfundisha Musa habari za Mungu na za watu wake.

Je! mimi ni nani?

Nilikuwa na mpango kwa maisha ya Musa. Ulikuwa mpango wangu kwake kutouawa na Farao. Ulikuwa mpango wangu kwake kuelimishwa katika makao ya mfalme. Ninao pia mpango kwa maisha yako.

Je! mimi ni nani?




1. Miriamu




2. Mamaye Musa



3. Musa



4. MUNGU



5. Binti Mfalme

Je! ni maneno gani katika maneno yafuatayo hapo chini yalifanyika kwanza? Andika namba kando yao kufuatana na wakati yalipotukia kwanza (kwa mfano, neno lililofanyika kwanza uandike namba 1 kando yake, la pili uandike namba 2, na kuendelea mpaka uyamalize).

—— Mamaye Musa alimficha nyumbani kwa miezi mitatu.

—— Binti Mfalme alimwokota akampeleka kukaa katika makao ya mfalme.

—— Farao aliamuru watoto wote wanaume wa Kiebrania kuuawa.

—— Mamaye Musa aliweza kumfundisha Musa habari za Mungu.

—— Musa alitiwa ndani ya kisafina cha manyasi, akawekwa kando ya mto. Miriamu alimlinda.

Je! unaweza kuona sasa jinsi Mungu alivyofanya kila jambo kwa kusudi la wema katika maisha ya Musa?

1. Mungu aliokoa maisha ya Musa baada ya Farao kuamuru auawe.
2. Alikaa katika makao ya mfalme.
3. Alifundishwa na kulelewa na mama yake aliyemzaa.
4. Alipata elimu nzuri.

Ikiwa unampenda Mungu, anaweza kufanya mema katika mambo yote maishani mwako.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema.”

Warumi 8:28



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Saba

MUNGU ASEMA NA MUSA

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 3:1-6

Musa alipokuwa mkubwa, alitamani sana kukaa na Waebrania, watu wake. Alijua ya kwamba itampasa kuacha maisha mazuri katika makao ya Farao pamoja na utajiri wake.

Siku moja alimwona Mmisri mmoja msimamizi akimpiga Mwebrania mtumwa. Musa alikasirika sana akamwua msimamizi yule. Alifikiri kwamba hapakuwapo mtu aliyekuwa akimwona, kwa hivyo alimficha ndani ya mchanga. Lakini kabla ya muda mrefu, kila mtu alikuwa akizungumza juu ya Musa. Wakati Farao aliposikia habari, aliamuru kwamba Musa auawe. Musa alikimbia kwenda Midiani na kuwaacha watu wake aliowapenda.

Nchi ya Midiani ilikuwa mbali sana na Misri. Baadaye Musa alioa, akachunga kondoo za mkwe wake. Alijifunza mambo mengi kuhusu nyika. Maisha hayo yalikuwa mapya kwake kwa sababu alikuwa hajawahi kukaa mbali na makao ya mfalme nchini Misri.

Musa alitumia wakati huu kuzungumza na Mungu. Kwa sababu alikuwa peke yake pamoja na kondoo za mkwe wake alizokuwa akichunga, alitumia nyakati nyingi sana kumsikiliza Mungu.

Siku moja, wakati jua lilipokuwa kali sana, Musa alikuwa akitembea na kondoo za mkwe wake akiwachunga. Alitamani sana kukaa na watu wake. Alifikiria jinsi walivyokuwa wakiteswa.

Ilikuwa kama saa sita mchana. Mahali pale Musa alipokuwapo palikuwa na miti mingi ya miiba. Mara alipofika karibu na mlima, kijiti kiliwaka moto chenyeuwe.

Musa alisogea karibu kuona kitu ambacho kiliwakisha kijiti kile moto. Hata alistaajabu sana kwa sababu kijiti kile kiliwaka moto lakini hakikuteke-tea. Sauti ya Mungu ilimwita kutoka katikati ya kijiti kile ikisema, "Musa! Musa!" (Kutoka 3:4)



Musa alistaajabu sana. Alijibu mara moja, "Mimi hapa." (Kutoka 3:4)

Mungu alisema tena na Musa. Alinwambia, "Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. Tena akasema Mimi ni Mungu...." (Kutoka 3:5-6)

Musa aliogopa sana akaficha uso wake asiweze kumwambia Mungu. Lakini Mungu aliendelea kusema. "Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri. ...Nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema." (Kutoka 3:7-8)

Kisha Mungu alimwambia Musa sababu ya kumtokea siku ile. "Haya, basi, nitakutuma sasa kwa Farao, ili upate kuwatoa watu wangu, hao wana wa Israeli, katika Misri." (Kutoka 3:10)

Wakati Musa alipokuwa akisikiliza, alijua kwamba Mungu alikuwa akimtararisha kwa kazi hii. Sasa angerudi kwa watu wake. Angesaidia kuwafanya kuwa huru.

KAZI YA KUFANYA:

Uganisha alama (au vitone) katika picha hii kuona jambo ambalo Musa aliona.



Jaza nafasi zilizoachwa kwa maneno ya kweli:

1. Baada ya Musa kukimbilia nchi ya Midiani, alichunga _____ za mkwe wake.
2. Mungu alimtokea Musa katika mfano wa _____ kilichowaka moto.
3. Mungu alimwambia Musa kuvua _____.

Andika herufi "K" kando ya sentensi ya kweli na uandike herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

- 1. Musa alitaka kukaa katika makao ya mfalme Misri maishani mwake mwote.
- 2. Musa alimwua Mmisri msimamizi kwa sababu Mmisri alimpiga Mwisraeli mtumwa.
- 3. Kijiti kile kiliteketea kabisa.

- 4. Mungu alimwambia Musa ya kwamba watu wake wangekuwa huru.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu.”

Zaburi 46:10

Sisi tukiwa kama Musa, tunahitaji kuwa tayari kumsikiliza Mungu. Mungu husema nasi mara kwa mara wakati tukiwa kimya katika mahali fulani peke yetu tukifikiria habari zake.

“Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.” (Isaya 6:8)

Katika andiko hili Isaya anamwambia Bwana ya kwamba atafanya kitu cho chote ambacho Bwana atamwambia kufanya. Sisi tukiwa kama Musa na Isaya, tunahitaji kuwa tayari Mungu kututumia.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI

KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Nane

KUTOKA MLIMA WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 20:3-4, 7-8, 12-17

Waisraeli walikuwa wamechoka kwa safari yao. Walikwisha kutembea mwendo mrefu sana kupitia jangwa. Walinung'unika na kuzungumza juu ya taabu yao wakati wote.

Hatimaye Musa aliwaongoza mpaka wakafika katika Mlima wa Sinai. Walipiga kambi yao chini ya mlima huo. Walifurahi sana kupumzika. Katika mahali hapa palikuwa na maji mengi na majani kwa ng'ombe, mbuzi, na kondoo zao.

Mungu ndiye aliyewaongoza watu hawa wake salama mpaka kufikia mlima huo. Aliwalinda na kuwapa chakula kwa safari yao.

Wakati kila mtu alipokwisha kupiga hema yake na kutulia, Musa alipanda mlima huo kuzungumza na Mungu. Alipokuwa juu ya mlima huo na kutazama chini yake, aliona hema zilizojengwa katika mistari, kondoo, ng'ombe, na watu.

Mungu alisema na Musa, akamwambia, "Waambie watu wangu kwamba nimewaokoa na kuwaongoza kutoka katika nchi ya Misri. Ikiwa watanitii mimi, watakuwa watu wangu maalum."

Musa alishuka mlimani, akawaita wazee wote pamoja, akawaambia maneno Mungu aliyoyasema. "Watu wote wakitika pamoja wakasema, Hayo yote aliyoyasema Bwana tutayatenda." (Kutoka 19:8a)

Musa alipanda tena mlimani. Mungu alimwambia, "Katika muda wa siku tatu nitakuja kusema na watu mimi mwenyewe. Nataka wao kunisikia na kuniona."

Wakati Musa alipowaambia watu habari hii, walianza kujitayarisha. Wengine walifagia hema, wengine walilisha mifugo, wengine waliteka maji, na wengine waliandaa chakula. Kila mmoja alioga kwa sababu walitaka kuonekana wasafi kwa Mungu.

“Ikawa siku ya tatu, wakati wa asubuhi, palikuwa na ngurumo na radi, na wingu nzito juu ya mlima, na sauti ya baragumu iliyolia sana. (Kutoka 19:16a) Musa alikwisha kuwaambia watu ya kwamba mambo hayo ndiyo yangukuwa ishara ya kuja kwa Mungu. Walikusanyika pamoja chini ya mlima kukutana na Mungu.



Mlima wa Sinai ulionekana kama kwamba ulikuwa ukiwaka moto. Moshi ulienea kila mahali. Musa alijua kwamba Bwana ndiye aliyeshuka mlimani katika moshi.

Kisha Mungu alisema na watu. Aliwapa sheria za kufuata. Tunaziita sheria hizi Amri Kumi za Mungu. (Unaweza kusoma Kutoka 20:3-4, 7-8, 12-17.)

Wakati Mungu alipomaliza kusema, watu walijua wazi kwamba Mungu ndiye waliyemsikia akisema nao. Waliogopa sana. Lakini Musa

aliwaambia, “Msiogope. Mungu amekuja kutufundisha jinsi ya kuishi maisha mema.”

KAZI YA KUFANYA:

Fuata mistari hiyo kuona kitu ambacho Mungu aliwapa Waisraeli.


A M

K M

Z A

N S O U

Chora mstari kutoka kwa picha ya kisafina hadi kwa mahali katika ramani inayoonyesha mahali ambapo Musa aliwekwa wakati alipokuwa mdogo. Chora mstari kutoka kwa mchungaji hadi mahali ambapo Musa alichunga kondoo. Chora mstari kutoka mlimani hadi mahali ambapo Musa alipokea Amri Kumi.



Weka alama hii (✓) kando ya sentensi ya kweli.

1. Wakati Waisraeli walipoondoka Misri

- Walisafiri kwa motakaa.
- Walitembea.
- Walisafiri kwa magari ya mfalme.

2. Wakati Mungu alipotoa Amri Kumi kwa watu wake

- Wote walipanda mlimani.
- Mungu aliwajia katika wingu na moshi.
- Musa aliwaambia watu kwamba haikuwa muhimu kusikiliza.

Katika maandiko ya somo hili, Amri Kumi zimeandikwa kulingana na jinsi zinavyofaa. Hapo chini ni tafsiri mpya ya amri hizi. Linganisha maandiko hayo na katika mistari iliyo kando ya

tafsiri hizo uandike namba kulingana na jinsi zinavyopasa kufuatana.

- Heshimu maisha ya binadamu.
- Fanya mambo ya uaminifu.
- Heshimu jina la Mungu.
- Mpende Mungu kuliko mambo yote.
- Fanya siku ya Jumapili kuwa tofauti na siku nyingine.
- Tii wazazi wako.
- Kuwa na fikira safi.
- Furahi na wengine katika mambo mema.
- Sema ukweli.
- Usiruhusu kitu cho chote kukutenga na Mungu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Sasa basi ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu....”

Kutoka 19:5

Kushika sheria ya Mungu ni muhimu sana. Wakati tunapomtii, tunampe-ndeza. Kisha tunakuwa sehemu ya watu wake maalum.

Je! utajaribu kushika sheria ya Mungu? Je! unataka kuwa mmojawapo wa watu wake maalum?



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Tisa

KUWASAIIDIA WENGINE

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo
24:15-20

Ilikuwa jioni. Ibrahimu alimwita Eliezeri, mtumishi wake aliyekuwa mwaminifu sana, kwake. Eliezeri alikuwa amekwisha kumtumikia Ibrahimu miaka mingi. Ibrahimu alikuwa mzee sana, na alikuwa na wasiwasi moyoni mwake.

Alimwambia Eliezeri, “Mwanangu Isaka anahitaji mke. Lakini haimpasi kuoa mke katika binti za Wakanaani. Binti za Wakanaani ni waovu na wanaabudu miungu badala ya kumwabudu Mungu wa kweli. Nataka uende mpaka nchi yetu ukamtwalie mwanangu Isaka mke.”

Eliezeri alisema, “Labda yule mwanamke hatakubali kufuatana nami mpaka nchi hii....” (Mwanzo 24:5) Lakini Ibrahimu alimwambia, Mungu atakusaidia kumpatia mwanangu mke na kuja naye.”

Kazi hii ilikuwa kubwa kwa Eliezeri mtumishi mzee. Labda angalitoa

udhuru mwingi kwa kutotaka kwenda. Alikuwa mzee na pengine hangeweza kusafiri siku nyingi kwa ngamia. Labda kungekuwa na joto jingi mchana na baridi nyingi usiku. Kando ya njia ambayo wangepitia kulikuwa na wezi wengi. Lakini Eliezeri hakutoa udhuru wo wote. Aliamuru ngamia kupakiwa mizigo kisha alichagua watumishi wengine ambao wangesafiri naye, wakaanza safari yao ndefu.

Baada ya kusafiri siku nyingi walifika katika kisima kilichokuwa karibu na mji ambako Ibrahimu alikaa zamani. Ilikuwa jioni na wanawake walikuwa wakija kisimani kuteka maji. Eliezeri aliomba, “Ee Bwana, nakuomba unisaidie. Nionyeshe msichana ambaye umemchagua kuwa mke wa Isaka. Mfanye anipe maji ninywe. Kisha awatekee ngamia zangu maji.”

Msichana mmoja aliyeitwa Rebeka alikuwa mmoja wa wasichana waliokuwako kisimani. Eliezeri alimwendea, akasema, “Tafadhali




unipe maji kidogo katika mtungi wako ninywe.” (Mwanzo 24:17b)

Rebeka alicheka kidogo, akatua mtungi wake mkononi mwake, akasema, “Unywe, bwana wangu.” (Mwanzo 24:18) Maji yale yalikuwa baridi.

Kisha Rebeka alisema, “Na ngamia zako nitawatekea, hata watakapo-kwisha kunywa.” (Kutoka 24:19)

Eliezeri alimshukuru Mungu moyoni mwake kwa sababu alijua kwamba msichana huyu ndiye Mungu alimchagulia Isaka kuwa mkewe.

Rebeka alifanya haraka, akamwaga maji ya mtungi wake katika birika, akapiga mbio kisimani kuteka maji



mengine. Watumishi pamoja na ngamia zao walikunywa maji mpaka wakatosheka. Ilikuwa kazi ngumu

kuteka maji kisimani lakini Rebeka alifurahi kushiriki maji na Eliezeri pamoja na watu wake waliokuwa na kiu na ngamia waliochoka.

Eliezeri alitambua kwamba babuye Rebeka alikuwa ndugu ya Ibrahimu. Alimwuliza Rebeka kama wangeweza kukaa kwao. Walikaribishwa vizuri sana wakaangaliwa karamu.

Eliezeri alieleza sababu iliyomfanya kuja. Wazazi wa Rebeka walisema, “Rebeka ataolewa na Isaka. Ni mpango wa Mungu.” Rebeka na watumishi wale walijitayarisha kurudi. Walisafiri siku nyingi.


Siku moja jioni walipofika katika konde moja, Rebeka alimwona Isaka akitembea peke yake. Alishuka juu ya ngamia, akatwaa shela yake akafunika uso wake. Alingojea Eliezeri kumwambia Isaka habari zake na za jamaa yake.

Eliezeri alijiharakisha kwenda kwa Ibrahimu kumwambia jinsi alivyom-pata Rebeka kisimani. Alimwambia jinsi Rebeka alivyowasaidia sana na jinsi alivyowaonyesha wema wake.

KAZI YA KUFANYA:



1. Eliezeri, mtumishi.



2. wazazi wa
Rebeka.



3. Rebeka.

Je! ni mtu au watu gani waliosaidia katika mojawapo au katika njia hizi zote? Kuna namba chini ya kila picha. Andika namba hiyo katika mojawapo ya mistari iliyo kando ya sentensi inayoonyesha wakati mtu huyo aliposaidia katika njia hizi.

- Alikwenda wakati alipotumwa.
- Alishiriki chakula, maji, na makao.
- Alifanya kazi iliyohitaji kufanywa.
- Alitimiza ahadi? Hakujaribu kuepuka wajibu wake?
- Alionyesha wema wake kwa wanyama.
- Aliwafanya wageni kukaribishwa vizuri.

— Aliomba uongozi wa Mungu.

Je! ninaweza kufanya nini kusaidia. Weka alama hii (✓) katika mistari iliyo kando ya mambo utakayojaribu kufanya.

- Nikitumwa nitakwenda kwa furaha.
- Nitashiriki chakula na maji.
- Nitatimiza ahadi.
- Nitawahurumia wanyama.
- Nitawakaribisha wageni vizuri.
- Nitaomba uongozi wa Mungu.

Jaza nafasi zilizozachwa kwa majibu yanayofaa.

1. Je! ni kazi zipi mbili zilizohitaji kufanywa?

2. Je! ni nani aliyeulizwa kufanya kazi hizi?

3. Je! kila mmoja alifanya kazi yake vyema? _____

4. Je! unafanya kazi zako vyema? _____

VIFUNGU VYA KUKUMBUKA:

"Amri yangu, ndiyo hii Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi."

Yohana 15:12

"...Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi."

Waefeso 4:32

"Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako...."

Mhubiri 9:10

Ni rahisi kwetu kusaidia na kuwa wema kwa watu wengine tunapowapenda, lakini ni vigumu sana kuwapenda watu kama hawatupendi. Yesu anatwamuru kupendana na kuwa wafadhili sisi kwa sisi.

Maneno "lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya" maana yake ni kazi ndogo zinazohitaji kufanywa kila siku kuteka maji, kuokota kuni, kuwasaidia ndugu na dada wadogo.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI

KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Kumi

MSHINDI WA AMANI

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo
26:12-33

Kulikuwa na njaa kubwa wakati wa Isaka. Kwa sababu ya njaa hii Isaka pamoja na jamaa yake na mifugo walihama, wakaenda kukaa katika nchi nyingine. Nchi aliyohamia iliitwa Gerari. Isaka alichimba visima katika nchi ile, alipanda mimea na alilisha mifugo yake pia. Alifanikiwa katika mambo yote aliyofanya na Wafilisti walianza kumwonea wivu. Mfalme wa nchi ile aliyeitwa Abimeleki alimwambia Isaka, "Utoke kwetu, maana wewe una nguvu sana kuliko sisi." (Mwanzo 26:16) Ingawa Isaka na watu wake walikuwa na nguvu nyingi zaidi kuliko Wafilisti, hakutaka kupigana vita nao. Ilikuwa vigumu sana kwa Isaka kuihama nchi ile na kuacha shamba na visima vyake, na kwenda kutafuta mahali pengine papyrus kukaa. Walakini Isaka alichukua jamaa yake, watumishi wake, na mifugo yake akahama.



Katika mahali hapa papyrus Isaka alipata visima vilivyochimbwa miaka mingi iliyopita. Visima hivi vilikuwa vimefukiwa kwa takataka na matope. Walivichimbua tena na maji yalianza kububujika. Walipomaliza kuvichimbua, wachungaji kutoka Gerari

walikuja, wakawaambia kwamba maji hayo ni yao.



Isaka aliwaambia watu wake kuchimba kisima kingine. Watu wake walifanya kazi kwa bidii kuchimba kisima kingine ambacho kilikuwa na kina kirefu. Walitaka maji mazuri. Wakati maji yalipoanza kububujika kisimani mle, wachungaji wa Gerari walikuja tena, wakadai kwamba maji hayo yalikuwa yao.



Isaka aliona kwamba watu wake walikuwa wamechoka. Mikono yao ilikuwa ikiuma. Migongo yao ilikuwa imechoka kwa kuchimba sana. Walakini aliwaambia kuchimba kisima kingine mahali pengine.

Walichimba kisima kingine ambacho walipata maji mazuri. Wakati huu hakuna mtu aliyegombana nao. “Bwana ametufanyia nafasi,” Isaka aliwaambia watu wake. Walimshukuru



Mungu. Mungu alimbariki Isaka na alimfanya kusitawi sana katika mahali pale.

Mfalme Abimeleki alimjia Isaka na kumwambia, “Hakika tuliona ya kwamba Bwana alikuwa pamoja nawe. Na tuapiane, na kufanya mapatano nawe...”

Isaka alihama mara nyingi kwa sababu alitaka amani. Sasa alifurahi kuapiana na mfalme kwamba wangepaa kwa amani. Isaka aliandaa karamu na wote wakala, wakanywa. Waliamka asubuhi na mapema, wakaapiana. Halafu Isaka aliwaruhusu kwenda zao kwa amani.

Siku ile baadaye, watumishi wa Isaka walikuja, wakampasha habari kwamba “Tumeona maji.” (Mwanzo 26:32b) Isaka alijiharakisha kwenda kuona kisima hicho. Alijua kwamba kisima hicho pamoja na visima vingine ambavyo wangepachika siku za baadaye vingewakumbusha watu kwamba ugomvi unaweza kumalizwa kwa njia ya amani.

Shida zetu pia zinaweza kumalizwa kwa njia ya amani kama tutafuata mapenzi ya Mungu na uongozi wake.

KAZI YA KUFANYA:

Andika herufi “K” kando ya sentensi ya kweli, na uandike herufi “M” kando ya sentensi ambayo si kweli.

- 1. Isaka alikuwa mshindi wa amani kwa sababu alikataa kugombana hata wakati mtu alipomkosea.

- 2. Isaka alikuwa na moyo wa kutosha vitu vilivyokuwa vyake ili aweze kuwa na amani.
- 3. Isaka alikuwa mpole wakati wengine walipokasirika.
- 4. Isaka alikuwa mwema kwa maadui zake.
- 5. Isaka alitaka vita kila siku.
- 6. Isaka alisuluhisha ugomvi bila mapigano.
- 7. Isaka alikataa kuhamia mahali pengine papya.
- 8. Isaka hakuwa mtu mkali.
- 9. Isaka hakupatana na watu wengine.
- 10. Isaka alionyesha kwamba ingawa alikuwa na utajiri mwingi, hakuhitaji kuwa katili au mwenye choyo.

Soma vifungu vifuatavyo, kisha ukamilishe sentensi zifuatazo.

_____ hugeza hasira; bali neno liumizalo huchochea _____. (Mithali 15:1)

Heri wenye upole; maana hao watairithi _____. (Mathayo 5:5)

Heri wapatanishi; maana hao wataitwa _____ . (Mathayo 5:9)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Jawabu la upole hugeza hasira; bali neno liumizalo huchochea ghadhabu.”

Mithali 15:1

Je! tunafuata mafunzo yanayoelezwa katika kifungu hiki? Wakati mtu anapotukasirisha, inatupasa kufikiri kabla kujibu. Tukifikiri kabla kujibu, tutaweza kujibu katika njia itakayoonyesha upendo wa Kikristo. Tukisema kwa hasira, maneno yetu yatawakasirisha watu wengine.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI

KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Kumi na Moja

KUJENGA TENA UKUTA

MASOMO YA BIBLIA: Nehemia 2:1-6, 13-18; 4:6; 6:15-16

Katika somo hili tutajifunza habari za mtu mmoja anayeitwa Nehemia. Mji wa Yerusalemu ulitekwa na watu wengi walikamatwa kama mateka wa vita. Walipelekwa katika nchi ya Babeli. Baadaye walitawaliwa na mfalme wa Uajemi. Nehemia alikuwa mmoja wa watu waliokamatwa mateka. Alifanywa kuwa mtumishi wa mfalme wa Uajemi.

Wakati alipokuwa Uajemi, wageni walimletea habari ya kwamba mji wa Yerusalemu uliharibiwa. Ukuta wake ulibomolewa na milango yote iliteketezwa. Nehemia aliposikia habari hii aliketi chini, akalia sana. Sisi sote tunapenda kijiji au mji wetu. Nehemia alimwomba Mungu msaada wake ili angeweza kuwasaidia watu wake.

Siku moja, wakati Nehemia alipokuwa akimtumikia mfalme, mfalme alimwuliza kwa nini alikuwa na huzuni nyingi. Aliogopa kujibu swali la mfalme lakini alijua kwamba ilimpasa



kusema ukweli. Alimwambia mfalme habari alizoambiwa kuhusu mji wao wa Yerusalemu, akamwomba mfalme kumruhusu kwenda kujenga tena ukuta wa Yerusalemu. Mfalme alimruhusu Nehemia kwenda Yerusalemu. Pia mfalme alimpa barua kwenda nazo. Barua moja ilikuwa ya kitambulisho ambayo angewaonyesha maliwali wa nchi ambazo angepitia. Kwa kufanya

hivyo hangeweza kukabiliwa na shida yo yote katika safari yake. Barua nyingine aliambiwa na mfalme kumpa mwenye kutunza mwitu wa mfalme ili mtunza mwitu huyo angeweza kumpa miti ya kujengea ukuta na milango ya hekalu.

Nehemia alisafiri kwenda Yerusalemu. Siku moja baada ya kuwasili kwake Yerusalemu, alitoka nje usiku kutazama kuta. Alipanga jambo ambalo angefanya. Aliwaambia watu mpango wa Mungu wa kujenga tena mji wa Yerusalemu. Walikubaliana naye kwa furaha. Walisema, "Haya! na tuondoke tukajenge." (Nehemia 2:18)

Palikuwa na watu watatu waliowadharau Nehemia na wafanya kazi. Walakini Nehemia na wafanya kazi hao waliendelea kufanya kazi kwa bidii kuujenga tena ukuta. Walifanya kazi kuanzia asubuhi hadi jioni. Pia iliwabidi kulinda ukuta usiharibiwe na watu waliotaka kuuharibu.

Watu wanapochoka kufanya kazi, wanaanza kutopatana. Jambo hili linaweza kuleta mgawanyiko ambao unaweza kuleta vita. Wafanya kazi pamoja na Nehemia walichoka sana kwa sababu walifanya kazi bila kupumzika. Nusu yao walisimama kulinda na nusu nyingine waliendelea kujenga ukuta. Wakati wa usiku hawakuvua nguo zao, bali walilala nazo. Walibeba silaha zao mikononi mwao kila wakati.

Wanawake walianza kunung'unika kuhusu hali yao ya kuishi. Wakuu wengi na maafisa walikuwa wakiwadanganya watu. Mashamba yao yalikuwa yakiwekwa rehani na watoto

wao walikuwa wakilazimishwa kufanya kazi kama watumwa. Nehemia alikasirika sana aliposikia habari hii. Aliwahukumu wakuu na maafisa hawa. Walimsikiliza, wakabadili njia zao mbaya za kushughulika na watu. Kisha watu walirudi kujenga tena ukuta kama walivyoahidi kufanya.

Watu kutoka nje ya Yerusalemu walijaribu kumvunja Nehemia moyo. Lakini Nehemia alimwomba Mungu nguvu apate kumaliza kazi ile na Mungu alijibu maombi yake.

Ilichukua siku hamsini na mbili kujenga tena ukuta wa Yerusalemu. Maadui waliposikia habari kwamba ujenzi ulimalizika, waliogopa. Wayahudi walijua kwamba walifanya vizuri kushirikiana pamoja kujenga ukuta. Sasa walikuwa salama kwa sababu ukuta huo uliwalinda kutokana na mashambulio ya maadui zao. Ukuta huo ulijengwa kwa sababu watu wote walikuwa na nia ya kufanya kazi pamoja.

KAZI YA KUFANYA:

Sisi sote tunahitaji kujifunza jinsi ya kufanya kazi vizuri. Pia tunahitaji kujifunza jinsi ya kufanya kazi pamoja na wengine. Wayahudi waliweza kujenga ukuta kwa sababu walikuwa "na moyo wa kutenda kazi" na walifanya kazi pamoja. Hawakufa moyo. Hapo chini utaona picha ya ukuta wa mawe. Katika kila jiwe kuna sentensi. Kila sentensi inasema jambo ambalo utataka kufanya ili kuwa mfanya kazi maalum. Jaza nafasi za kila sentensi. Sentensi kamili zimeandikwa chini ya ukuta na

zitakusaidia kujua maneno ya kujaza
katika nafasi hizo.

2. Nitaifunza ya kufanya kazi hiyo.	1. Ninapopata kazi ya kufanya ninaifanya kama ninavyo- weza.	3. Kazi hiyo ni ngumu, lakini kufanya.
4. Ningependa kufanya kazi nyingine, lakini nitafanya hii kwa sababu kufanywa.		
5. Ni kazi ngumu, lakini tukishirikiana pamoja kuifanya.		6. Ninapopewa kazi ya kufanya

Andika majibu katika nafasi
zilizoachwa katika mchezo huu wa
fumbo. Andika herufi moja tu katika
kila chumba.

	1.								
2.									
	3.								
	4.								

1. Je! ni mji gani uliokuwa na ukuta
uliobomolewa? (Andika kutoka juu
mpaka chini.)
2. Je! ni nani aliyekata shauri kujenga
tena ukuta?
3. Baada ya ukuta kujengwa, watu
waliweza kulala _____.
4. Je! ni nani aliyewasaidia watu
kujenga ukuta?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

**"Maana sisi tu wafanya kazi pamoja
na Mungu."**

1 Wakorintho 3:9a

Kwa sababu watu walikuwa na moyo
wa kutenda kazi pamoja iliwachukua
siku hamsini na mbili kumaliza kujenga
ukuta wa Yerusalemu. Wayahudi
wafanya kazi walishirikiana pamoja na
walishirikiana na Mungu pia.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI

KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Kumi na Mbili

JINSI YA KUSAMEHE

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 6:14-15; 18:21-35

Je! unajua Sala ya Bwana kwa moyo? Ikiwa unajua sala hii, utakumbuka kwamba maneno haya yanapatikana ndani: "Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu." (Mathayo 6:12) Je! maneno haya yana maana gani? Tunaweza kujifunza kutoka kwa Yesu maana ya maneno haya kama Petro alivyofanya.

Petro alimwuliza Yesu, "Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? hata mara saba?" (Mathayo 18:21) Petro alifikiri kwamba alijua jibu la swali lake. Alifikiri kwamba kumsamehe mtu mara saba kulitosha.

Yesu hakukubali jibu la Petro. Alimwambia, "Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini." (Mathayo 18:22) Yesu alitaka Petro kujua kwamba hatuhesabu mara kadha tunapomsamehe mtu, bali tunamsamehe mara nyingi kama inavyohitajika.

Labda Petro alikuwa bado kumsamehe mtu ye yote mara saba, na sasa Yesu alikuwa akimwambia asamehe saba mara sabini.

Baadaye Yesu alisimulia hadithi moja kuyafanya maneno yake kufahamika zaidi. Alisimulia hadithi ifuatayo: Hapo kale palikuwa na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. Alitambua kwamba mtumwa wake mmoja alikuwa na deni lake zaidi ya shilingi milioni moja. Mtumwa yule hangeweza kulipa deni hilo.

Mfalme aliamuru kwamba mtumwa yule auzwe, yeye na mkewe na watoto wake. "Uzeni vitu vyake vyote mnilitee pesa mtakazopata," mfalme alisema.

Mtumwa yule alimsihi sana mfalme, akasema, "Bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia." (Mathayo 18:26)

Mfalme alimhurumia sana. Alimfungua, akamsamehe deni lile. Wakati mtumwa yule alipokuwa njiani kurudi nyumbani, alikutana na mjoli

wake aliyemwia shilingi 300. Alimwambia, "Nilipe uwiwacho." (Mathayo 18:28)

Mjoli huyo wake alimsihi akisema, "Nivumilie, nami nitakulipa yote pia." (Mathayo 18:29)

Mtumwa yule hakumhurumia mjoli wake, bali alisema "Mfungeni mtu huyu gerezani mpaka atakaponilipa deni iangu lote."

Watumwa wengine walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana. Walikwenda kwa mfalme, wakamweleza mambo hayo yote.

"Mleteni kwangu," mfalme aliamuru. Alipoletwa, mfalme alimwambia, "Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi; nawe, je! haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe?" (Mathayo 18:32-33) "Sasa utafungwa gerezani mpaka utakaponilipa deni langu lote."

Wakati Yesu alipomaliza kusimulia hadithi hiyo, alimgeukia Petro, akamwambia, "Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi; msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake." (Mathayo 18:35)

KAZI YA KUFANYA:

Je! ninataka kuwa mtu wa namna gani?

Jifunze sentensi hapo chini kwa uangalifu. Weka alama hii (✓) kando ya sentensi zinazoeleza namna ya mtu unayotaka kuwa:

— Yule anayekumbuka kosa analotendewa na wengine.



— Yule anayewasamehe wengine makosa yao.

— Yule anayejaribu kuwakosea wale wanaomkosea.

— Yule hakasiriki mara moja.

— Yule anayekataa kuwasamehe wengine.

— Yule anayependa kulia na kwenda nyumbani wakati mambo yanapofanyika katika njia asiyopenda.

— Yule asiyejali hasira ya mwingine.

— Yule anayewachukia wengine.

— Yule anayesahau mambo yaliyopita.

— Yule anayewakumbusha wengine juu ya matendo yao mabaya.

Je! unaweza kufanya nini kuwa kama unavyotaka? Itakuwa vema kuomba juu ya jambo hili na kumwomba Mungu kukupa msaada wake.

Uganisha alama ndogo unazoziona hapo chini. Baada ya kufanya hivyo, ufikirie jibu la swali hili: Je! niko tayari kuwasamehe wengine mara nyingi sana?



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi.”

Mathayo 6:14

Ni lazima kuwasamehe watu wengine ikiwa tunataka msamaha wa Mungu. Tukiangalia orodha iliyo chini ya “Kazi ya Kufanya”, tunaona kwamba mtu mwenye msamaha ndiye mtu tunayepaswa kufuata mfano wake, na Mungu anatutaka sisi kuwa kama yeye.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI

KITABU CHA PILI

MUNGU ATUONYESHA NJIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2-2Ps

Sura ya Kumi na Tatu

MFUNGWA ASHUKURU

MASOMO YA BIBLIA: Wafilipi
1:1-11; 2:19-30; 4:10-20

Je! ni vigumu kwako kuwashukuru watu ambao wamekufanyia jambo fulani? Je! umepata kuwaandikia watu fulani kuwashukuru kwa mambo fulani mema waliyokufanyia?

Mmisheni Paulo aliandika barua ya shukrani. Wakati alipoanza kuandika barua hiyo, hakuwa akikalia kiti nyumbani mwake huko Tarso. Wakati huo Paulo alikuwako mjini Rumi katika nyumba ambayo Wakristo wenzake walimpa. Lakini hakuwa huru kutoka nyumbani mle. Alikuwa amefungwa kwa minyororo pamoja na askari mlinzi. Askari huyo mlinzi alikuwa mmojawapo wa askari wa mfalme Kaisari (Nero). Paulo alifungwa kwa sababu alikuwa Mkristo.

Ingekuwa vigumu sana kwetu kufurahi kama tungekuwa wafungwa. Lakini Paulo hakuketi na kusikitikia hali yake. Aliandika barua kwa marafiki zake wa kanisa la Filipi


kuwashukuru kwa mambo yote waliyokwisha kumfanyia.

Paulo alizoea mateso aliyopata wakati alipokuwa Rumi. Kaisari (Nero) alikuwa mtawala mwovu ambaye wakati mmoja aliamuru kwamba Wakristo wengine watupwe katika tundu la wanyama wakali na kuraruliwa au wauawe kwa upanga. Nero alikuwa amesema kwamba angemleta Paulo Rumi kuhukumiwa, lakini alingojea kwa miaka miwili kabla ya kufanya hivyo.

Paulo hakujitetea mwenyewe kwa njia yo yote. Wala hakuwaogopa askari au mtu ye yote. Alikuwa mvumilivu sana. Alijiingiza katika shughuli ya kuwasaidia wengine. Alimshukuru Mungu.

Ingawa nyumba ambayo Paulo alikaa ilikuwa ndogo, ilikuwa kama makao ya mfalme ikilinganishwa na ngome ambalo wafungwa wengine walikuwa wakifungwa. Nyumba hiyo ilikuwa na nafasi ya kumtosha Paulo

kutembea kunyosha miguu yake. Wakati wa mchana aliwafundisha watu waliokuja kumtembelea; na wakati wa usiku alikumbuka rehema za Mungu na kumshukuru.



Kwa sababu Paulo alikuwa amefungwa pamoja na askari mlinzi, askari huyo hakuweza kuondoka wakati Paulo alipoanza kufundisha habari za Mungu mmoja wa kweli na habari za Mwanawe ambaye ni Mwokozi wa ulimwengu. Paulo alimshukuru Mungu wakati alipotambua ya kwamba Injili aliyohubiri iliwafanya watu wengi kumjia Yesu.

Marafiki wengine wa Paulo waliacha kumtembelea wakati alipokamatwa na kufungwa. Labda walimwogopa Nero. Lakini Timotheo aliendelea kuwa mwaminifu kwa Paulo. Alizungumza naye juu ya upendo wa Mungu na ulinzi wake. Paulo hakuweza kuona vizuri. Labda Timotheo ndiye aliyemwandikia Paulo barua kwa Wafilipi. Mara nyingi Paulo alimwambia Timotheo, “Kanisa la Filipi ndilo kanisa la kwanza nililoanzisha Makedonia. Sitasahau ukarimu wa Wakristo wa kanisa hili. Nakumbuka chakula kizuri nilichopewa na Lidia wakati nilipokuwa mgeni nyumbani mwake. Nakumbuka misaada niliyotumiwa na kanisa lile wakati nilipohitaji.” Timotheo alimsikiliza Paulo kwa

uangelifu. Furaha ya Paulo ilikuwa ya moyo. Ilikuwa furaha ambayo ilionekana hata wakati wa taabu.

Siku moja Timotheo alikwenda mbio kwa Paulo, akamwambia, “Umetumiwa barua kutoka Filipi. Epafrodito yupo hapa, ameileta barua hiyo pamoja na zawadi.” Paulo alitokwa machozi lakini machozi hayo hayakuwa machozi ya huzuni. Yalikuwa machozi ya furaha. Alimkumbatia Epafrodito, kisha alimshukuru Mungu kwa zawadi zile. Alimwomba Epafrodito kumwambia habari zote za Wakristo wa Filipi.


Epafrodito alikaa na Paulo kwa muda. Siku moja alikuwa mgonjwa sana hata alikuwa karibu kufa. Mungu alimhurumia, na baada ya siku nyingi alikuwa mzima tena. Wakati alipoweza kusafiri, alirudi kwa kanisa lao la Filipi.

“Nenda kwa amani,” Paulo alimwambia Epafrodito. “Chukua barua hii ya shukrani uwapelekee Wakristo wa Filipi.” Kisha mmisheni Paulo alimpigia Epafrodito kwa-heri.

Epafrodito aliwapa Wakristo wa Filipi barua hiyo ya Paulo. Watu hao wa Filipi walitambua jinsi Paulo alivyokuwa na shukrani kwao na kwa mambo yote waliyomfanyia.

KAZI YA KUFANYA:

Baada ya kusoma somo hili na vifungu vya Biblia, andika vitu ambavyo Paulo alishukuru kwa ajili yao. Picha iliyopo hapo chini imefanana na barua ya Paulo. Andika majibu kama barua.



Andika vizuri maneno hayo hapo chini ili yaweze kusomwa. Unapomaliza kuyaandika, utaona kwamba Paulo alikuwa mtu wa namna gani.

**PALOU ALIWAKU UMT
NYEMWE SHURAKNI**

Hapo chini kuna sentensi kuhusu somo hili letu. Andika herufi “K” kando ya sentensi iliyo kweli, na uandike herufi “M” kando ya sentensi ambayo si kweli.

- Kifungu cha kukumbuka kiliandikwa na Paulo.
- Mwandishi wa kitabu cha Wafilipi alikuwa Paulo.
- Kitabu cha Wafilipi kinatufundisha umuhimu wa kushiriki vitu vyote sisi kwa sisi.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.”

1 Wathesalonike 5:18

Je! tunakumbuka kuwashukuru marafiki zetu kwa mambo wanayotufanyia? Je! tunakumbuka kuwashukuru wazazi wetu kwa mambo yote wanayotufanyia?

Je! tunakumbuka kumshukuru Yesu Kristo kwa vitu vyote tulivyo navyo, na kwa uhai wake aliooa msalabani ili tuweze kuokolewa katika dhambi zetu?